

Wapendwa Wazazi na Watunzaji,

Mtoto wako amepata ujuzi wa ufahamu wa fonolojia, na hivyo kumwezesha kutambua na kutumia sauti za lugha. Shughuli hizi zinazingatia sehemu ambazo mtu husikiza na sauti katika maneno. Tungependa kuendeleza masomo haya wakati wa likizo ya msimu wa baridi kupitia shindano! Mtoto wako amelikwa kujiunga na Shindano la Winter Heggerty; pata maelezo hapa chini

Kwa nini ufahamu wa fonolojia ni muhimu?

Ufahamu wa fonolojia ni kiashiria thabiti cha mafanikio ya usomaji, haswa katika hatua za mwanzo za ukuzaji wa usomaji, na hutumika kama msingi wa kusoma.

Ninawezaje kusaidia katika ufahamu wa fonolojia nyumbani?

Ni rahisi sana kusaidia katika ufahamu wa fonolojia—unachohitaji ni lugha! Msaidie mtoto wako kuelewa kuwa maneno anayosikiza katika unenaji huundwa na sehemu na sauti. Unaweza kuanza kukuza ufahamu wa fonolojia wa mtoto wako kwa kumruhusu atazame mafunzo yetu ya video ya ufahamu wa fonimu ya dakika 10 hadi 20.

Tunawezaje kupata rekodi hizo za mafunzo?

Tumia msimbo husika wa QR hapa chini ili kufikia rekodi za mafunzo kulingana na gredi ya mtoto wako.

Tunatazamia kuendelea kumsaidia mtoto wako katika kukuza ujuzi wa msingi wa kusoma na kuandika, na tunatumai mtoto wako atashiriki katika mafunzo yetu ya video wakati wa likizo!

Watoto wanaotazama video na kurudisha kumbukumbu (inayopatikana chini ya barua hii) wataingizwa kwenye shindano la bahati nasibu ya zawadi za mtu binafsi na za darasa.

Video za Shule ya Mapema	Video za Shule ya Chekechea	Video za Shule ya Msingi (Gredi za 1-2)
 https://rb.gy/9cv8g3	 https://rb.gy/2pbxtw	 https://rb.gy/14uwi7

Rudisha
kwa
mwalimu
wako
baada ya
likizo!

Jina la Mwanafunzi:		Kiwango cha Gredi:	Jengo:
Somo		Saini ya Mzazi	
Wiki ya 11	Siku ya 1		
	Siku ya 2		
	Siku ya 3		
	Siku ya 4		
	Siku ya 5		
Wiki ya 12	Siku ya 1		
	Siku ya 2		
	Siku ya 3		
	Siku ya 4		

